**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**
*(Barua zote ziandikwe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

**MKOA WA KILIMANJARO**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P. 176,
**MWANGA.**

Simu Na: 0272974343
: 0222974344
*E.Mail* *ded@mwangadc.go.tz*
*Web site:* *www.mwangadc.go.tz*

***Unapojibu tafadhali taja:***
Kumb. Na. **L.10/6/VOL.II/153**

20 Juni, 2025

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga anatangaza nafasi kumi na tano (15) za ajira ya muda ya kukusanya Ushuru / Mapato na nafasi kumi na tano (15) za Migambo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

### SIFA ZA MWOMBAJI – MKUSANYA USHURU / MAPATO (NAFASI 15)

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne / sita.
- Awe na Elimu ya kuanzia stashahada (diploma) na kuendelea kwenye fani ya biashara / uhasibu
- Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji
- Awe mkazi wa Mwanga

### MAJUKUMU YA WAKUSANYA USHURU / MAPATO

- Kukusanya mapato
- Kubaini vyanzo vya mapato
- Kuwa kwenye kituo chake cha kazi wakati wote
- Kuhakikisha hakuna uvujaji wa mapato ya Halmashauri
- Kazi zingine zote atakazopangiwa na mwajiri.

### SIFA ZA MWOMBAJI – MGAMBO (NAFASI 15)

- Awe amehitimu elimu ya Darasa la Saba na kuendelea.
- Awe amepitia mafunzo ya Mgambo na ana 'Force Number'
- Awe na Afya njema (Mkakamavu)
- Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji
- Awe mkazi wa Mwanga

## MAJUKUMU YA MGAMBO (ASKARI WA JESHI LA AKIBA)

- Kusimamia usalama wa mapato, watumishi na wakusanya mapato.
- Kulinda vyanzo vya mapato
- Kuhakikisha hakuna uvujaji wa mapato ya Halmashauri
- Kuwepo kwenye kituo cha kazi wakati wote.
- Kuwa tayari kufanya kazi muda wowote atakaohitajika.
- Kuhakikisha anafanya makabidhiano ya lindo endapo atapangiwa kituo cha kulinda.
- Kushirikiana na Mkusanya mapato kuzuia uvujaji wa mapato.
- Na kazi zingine zote atakazopangiwa na mwajiri.

## MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wawe na umri kati ya miaka 18 hadi miaka 40.
ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
iii. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yatakayojitosheleza (detailed c.v) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina yao.
iv. Maombi yote yaambatane na cheti cha kidato cha nne, sita na taaluma.
v. Awe na kitambulisho cha mpiga kura, cha taifa au namba ya kitambulisho.
vi. Picha mbili"passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
vii. Waombaji wenye ujuzi wa kutumia computer na wenye fani za udereva na wenye pikipiki binafsi watapewa kipaumbele zaidi.
viii. Awe anaweza kutumia simu janja (smart phone).
ix. Awe na wadhamini wawili.
x. Maombi yote yawasilishwe masjala ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia anwani ifuatayo;

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA,**
**S.L.P 176,**
**MWANGA.**

xi. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **26/06/2025** saa **9:30 Alasiri.**

Zahara A. Msangi,
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MWANGA

**Nakala:**

- Mbao zote za Matangazo.

- Katibu Tawala Mkoa,
  S. L. P 3070,
  **Moshi – Kilimanjaro.**

- Kata zote,
  **Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.**